



Mipangilio ya Makazi kwa watu wazima:


Wafanyakazi wa SWIS hufanya kazi kwa karibu sana na Wafanyakazi wa MCAF kuwahudumia wageni watu wazima. Kwa kutumia mfano wa usimamizi wa hoja, watumishi wa upande wa makazi hutoa musadaa na huduma kwa mgeni binafsi na familia zikaazo na kujiimarisha katika jamii.

SWIS huunganisha familia ya wageni na kitengo cha MCAF kinachokusika na mipangilio ya makazi kama:

- Masomo ya Lugha katika Lugha mbili rasmi za New Brunswick
- Huduma za watoto
- Wahusika wa Utamaduni
- Makundi ya kusaidia jamii mbalimbali (wanawake, wababa, vijana, shughuli za malezi nk.)
- Huduma za Ajira na Mafunzo
- Mafunzo na warsha

Ushirikiano na jamii

Timu ya SWIS inashirikiana na wanafunzi wapya, wazazi, shule za Kiingereza, mashirika na washirika ili kuwezesha mafanikio ya makazi na kuimarika kwa wageni katika Shule za Kiingereza, utamaduni na jamii.



Pamoja
Tutaendelea zaidi!

Shirika la Utamaduni la Fredericton Inc.


28 Barabara ya Saunders
Fredericton,
New Brunswick Canada E3B 1N1

Barua pepe: mcaf@mcaf.nb.ca

Simu: (506) 454-8292

Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada
Financé par: Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

Canada



Watumishi kuhusu Makazi katika mipangilio ya shuleni



www.mcaf.nb.ca

Wafanyakazi wa Shirika la Mchanganyiko wa Utamaduni la Fredericton (MCAF) hukakisha ya kuwa wanafunzi wageni na wazazi wanafahamu haki zao za kuchagua mfumo wa elimu ya Kifaransa au mfumo wa elimu ya Kiingereza hapa New Brunswick.

Watumishi kuhusu Makazi MCAF katika mipangilio ya shuleni (SWIS)

hutoa huduma za makazi kwa wanafunzi wavya na familia zao zinazoishi Fredericton na maeneo ya karibu ambao huchagua shule za Kiingereza au shule za kingereza zinawafunza na Kifaransa. Kwa kushirikiana na shule za maeneo wanayoishi, washirika na jamii wa Shule za Kiingereza Wilayani, wafanyakazi wa SWIS huwasaidia wanafunzi kujifunza na kujisikia vyema katika jamii na mazingira ya shule yao mpya.

Malengo ya Mipangilio ya SWIS

- Kutoa msaada kwa wageni na kurahisisha mafanikio kwenye makazi yao, ustawi na ushirikiano katika shule na jamii za Kiingereza
- Kutoa huduma zivutiazoo kiutamaduni kwa wanafunzi wageni, familia zao, wafanyakazi wa shule na washirika wa jamii
- Kuunga mkono jitahada za kuinua maendeleo na kupanua ujuzi wa lugha ya Kiingereza na Kifaransa na kukuza Fredericton kwa kuptia uhamiaji
- Kushirikiana na washirika wa jamii kwa kukuza utofauti na kushirikishwa kwa watu wa aina mbalimbali katika shule na jamii



Watumishi wa SWIS wanafanya nini katika shule za Kiingereza ?

■ Awamu ya 1: Mwelekeo

- Kusaidia wanafunzi wageni katika mchakato wa usajili wa shule
- Ziara za shule na mwelekeo kwa wanafunzi na familia
- Kutoa maelezo kwa ujumla ya shule na elimu ihusianayo na mipango ya ziada ya jamii
- Kufanya ukaguzi wa mahitaji kwa kila mwanafunzi na familia



■ Awamu ya 2: Baada ya kujiandikisha

- Kushirikiana na wafanyakazi wa shule na washirika wa jamii kwa kuhakikisha ya kwamba mahitaji ya wanafunzi wageni na familia ngeni yamejulikana, yametatuliwa na wamesaidiwa
- Kufuatilia mara kwa mara wanafunzi katika shule zao mpya ili wasaidiwe katika mchakato wa makazi na kujiimarisha
- Kuwasaidia wanafunzi na wazazi kuhusu vipindi vya maelekezo kwa lugha ya Kiingereza, Kifaransa au katika lugha yao asili
- Kusaidia kuwaandikisha na kuwashirikisha watoto na vijana wageni katika:
 - Mafundisho na kazi za shuleni baada ya muda wa shule
 - Programu ya MCAF baada ya ratiba ya shule
 - Mchanganyiko wa utamaduni katika kambi mbali mbali zinakuwepo kipindi cha kiangazi na katika program nyingine zinazokuwepo kipindi cha kiangazi.